

SABABU ZA UTEUZI POTOFU WA SINONIMU: MIFANO KUTOKA KISWAHILI

E. K. F. Chiduo

1.0 Utangulizi

Nadharia za mahusiano ya maneno kimaana zinaeleza kuwa kama maneno mawili au zaidi yanaweza kujitokeza au kutumiwa katika mazingira yale yale bila kuleta maana tofauti basi maneno hayo ni sinonimu. Maneno yanayojidhihirisha hivyo hayasababishi utata mkubwa kimatumizi. Lyons (1968), anauita uhusiano wa namna hii ni uhusiano wa sinonimu kamili. Singh (1982) anaafiki hoja kuwa sinonimu kamili si rahisi kupatikana katika lugha asilia kwani maneno mawili yanaweza tu kuwa sinonimu kamili iwapo tu yanaweza kutumiwa katika mazingira yale yale bila ya kubadilisha maana. Hata hivyo anahitimisha kwa kusema kuwa ni vigumu kupata maneno mengi ya aina hii katika lugha.

Uteuzi potofu wa baadhi ya sinonimu za Kiswahili ni utumiaji wa sinonimu ambazo haziakisi maana halisi inayokusudiwa na msemaji au mwandishi yaani maana inapotoshwa kwani haiwasilishi dhana ile iliyokuwa inakusudiwa na mzungumzaji au mwandishi.

Kuna sababu kadhaa zinazofanya uteuzi potofu wa sinonimu. Moja ya sababu hizo inatokana na neno moja kuwa na maana zinazohusiana na neno lingine. Hii ina maana kuwa neno moja kuwa na baadhi ya maana ambazo pia zipo katika neno lingine.

Sababu nyingine ni upotofu katika kuingiza sinonimu katika kamusi yaani neno linaingizwa ndani ya kamusi na kufasiriwa kwa njia ya sinonimu na sinonimu hizo kuchukuliwa kuwa ni sinonimu kamili wakati ambapo pengine si sinonimu kamili. Pia inapotokea kuwa na sinonimu nyingi yaani msururu mrefu wa sinonimu katika kidahizo kimoja ambazo hufikiriwa kuwa msururu huo ni sinonimu kamili za kidahizo husika ambapo pengine katika msururu huo vingine si sinonimu kamili. Kunapokuwa na Maana zinazokinzana ndani ya kitomeo cha kamusi zinaweza kuwa chanzo cha upotofu wa matumizi ya sinonimu. Sababu ya mwisho itakayojadiliwa kwa mujibu wa makala haya ni kanuni mbaalimbali za uzalishaji maneno zinavyoweza kuwa kikwazo na kusababisha upotofu katika matumizi.

Makala haya yanakusudia kufafanua sababu zinazomfanya msemaji au mwandishi akatumia neno lisilosahihi katika maandishi au mazungumzo. Makala inadondoa mifano kutoka TUKI (1981 na 2004) na Mohamed na

mwenzake (1998) ikionyesha jinsi kamusi hizo zilivyoingiza baadhi ya vitomeo vinavyoweza kuwakanganya watumiaji. Pamoja na kufafanua sababu za uteuzi potofu, makala itaonyesha namna ya kurekebisha hali hiyo.

2.0 Sinonimu katika Kamusi

Kamusi ni kitabu cha maneno ambacho watumiaji wa lugha hurejea ili kupata maana na matumizi ya maneno. Hartmann (1983) anasema kuwa taarifa za maana za maneno ndizo muhimu na ndizo zinazohitajiwa na watumiaji wengi.

Sinonimu ni maneno ambayo yana maumbo tofauti lakini maana yao ni moja (Jackson, 1988, Weinreich, 1975 na Singh, 1982). Kwa mfano:

mjane *nm (wa-)* 1 mtu asiyekuwa na mke au mume kwa kuachwa au kufiwa. 2 mtu ambaye hajaoa au kuolewa; mseja (TUKI (2004) uk. 248).

mseja *nm (wa-)* mtu ambaye hajaoa au kuolewa ingawa ameshafikia umri wa kufanya hivyo; mjane, mhuni (TUKI (imeshatajwa uk. 273). Maneno haya yameingizwa kama sinonimu zisizo kamili na ndiyo maana maelezo yametolewa kwanza kabla ya **sinonimu** kuonyeshwa. Hali hii inajidhihirisha tunapojaribu kuchanganua baadhi ya nduni za maneno hayo:

mjane	mseja.
[+binadamu]	[+binadamu]
[+mtu mzima]	[+mtu mzima]
[+oa]	[-oa]
[+ achwa] au	[-achwa]
[+kifo cha mwenzi]	[-kifo cha mwenzi]
[+pweke]	[+ pweke]

Maneno haya yanatofautiana katika nduni zake kadhaa. Wakati neno **mjane** lina nduni ya [+oa], **mseja** lina [-oa]. Katika **mjane** kuna [+kifo cha mwenzi] au [+kuachwa]. Katika neno **mseja** kuna [- kifo cha mwenzi] au [- kuachwa].

Hivyo kwa vile maneno haya mawili nduni zake zote si sawa hayakubaliki kuwa sinonimu kamili bali sinonimu zisizo kamili kwani si katika mazingira yote neno **mseja** linaweza kuchukua nafasi ya neno **mjane** na kinyume chake.

Hivyo mtumiaji kamusi sharti awe makini kubainisha tofauti zilizopo kati ya maneno kama haya ili kumwezesha kufanya uteuzi mwafaka wa maana anayoikusudia.

Kuna maneno katika kamusi ambayo yamefasiriwa kwa kutumia sinonimu tu bila ya maelezo. Hii ina maana kwamba maneno ya aina hiyo ni sinonimu kamili. Sinonimu kamili ni maneno ambayo nduni zake zote ni sawa na huweza kupishana nafasi bila ya kubadili maana katika mazingira yote. Katika kitomeo cha mfano hapa chini neno moja limeelezea neno lingine bila maelezo ya ziada. Kwa namna yalivyoingizwa katika TUKI (imeshatajwa 2004) tuangalie mfano wa neno **bwache** lilivyoingizwa katika kamusi hiyo:

bwache nm. mchicha, mdwere TUKI (imeshatajwa uk. 36).

Kwa namna ya uingizaji wa neno **bwache** na jinsi lilivyotumia neno **mchicha** kulifasiri inadhihirisha kuwa matumizi yake ni sawa mara zote. Hata hivyo ingawaje neno **mchicha** limefasiri neno **bwache** kwa hakika neno **mchicha** ni pana zaidi kimatumizi kwani kuna fahiwati za **mchicha** ambazo hazipo katika maana ya **bwache**. Tazama mifano ya matumizi ifuatayo:

- (i) Imemlazimu kutoa **mchicha** ili aweze kupata kazi.
- (ii) *Imemlazimu kutoa **bwache** ili aweze kupata kazi.

Katika mfano huo neno mchicha limetumika kwa maana isiyohusiana na majani ya mboga bali inayohusu utoaji wa rushwa au kitu kidogo ili mtu aweze kutimiziwa shida yake. Hivyo katika mazingira hayo ya matumizi maneno hayo si visawe.

Kitomeo **mchicha** kimeingizwa na kufafanuliwa ifuatavyo:

mchicha nm mmea ambao majani yake hupikwa na kuwa mboga; mdwere, bwache. TUKI (imeshatajwa uk. 235)

Hapa maana ya **mchicha** ni pana zaidi kwani katika litomeo hiki neno **mdwere** limeongezwa. Maneno haya matatu **mchicha**, **mdwere** na **bwache** yana uhusiano wa karibu na jinsi yalivyoingizwa katika KKS inaonyesha kuwa ni sinonimu kamili kulingana na maana za msingi. Hata hivyo uchanganuzi wa kina unaonyesha kuwa neno **mchicha** lina maana za ziada kama inavyojidhihirisha katika mfano wa hapo juu.

Kidahizo **mdwere** kimeingizwa na kufafanuliwa kwa sinonimu **mchicha** na **bwache** kama inavyoonyeshwa hapa chini:

mdwere nm (mi-) mchicha, bwache. TUKI (imeshatajwa uk. 238)

Sinonimu kamili zinajibainisha katika kamusi kwa kuingizwa kama maana peke yake ya kidahizo bila kuwa na maelezo ya ufafanuzi kama katika mifano ya **mdwere** na **bwache** hapo juu. Sinonimu zisizo kamili hutanguliwa na maelezo ya fasiri na ndipo sinonimu hutolewa kama katika mifano ya vitomeo za **mjane** na **mseja** hapo juu.

2.1 Msururu wa Visawe

Baadhi ya kamusi zimeorodhesha sinonimu zinazofikia 30 kwa kidahizo kimoja. Katika Mohamed . na mwenzake (1998) neno **madhila** limepewa sinonimu zifuatazo:

madhila n. mateso, taabu, unyonge, adha, shabuka, uonevu, ikabu, adhabu, takilifu, mushkili, usumbufu, maudhi, udhia, matatizo gubu, mashaka, ugumu, uzito, janga, uharabu, ginginizo, shakawa, shida, jakamoyo, masumbufu, idhilali, mzingile, jekejeke, kero, gingizo.

Msururu wa maana za kidahizo **madhila** ni mrefu mno kiasi unatia mashaka kwamba maneno hayo yote yana maana moja, yaani neno moja linaweza kutumika badala ya lingine na maana yake ikabaki ile ile. Jackson (1988) na wengine wana mashaka kwamba sinonimu halisi hazipo kwa wingi katika lugha ama sivyo hupunguza ufanisi na kuwa anasa katika lugha. Ndiyo maana tuna wasiwasi iwapo **madhila** ina sinonimu zote hizi. Mtumiaji asipokuwa makini anaweza kudhani kuwa maneno yote hayo yanaweza kuachiana nafasi bila ya kuathiri maana. TUKI (imeshatajwa 2004) imelifasiri neno **madhila** kama ifuatavyo:

madhila nm hali ya kuonewa au kuteswa; mateso, tabu
TUKI (imeshatajwa uk. 214).

Hapa tuchunguze baadhi ya sinonimu za neno **madhila** namna zilivyoingizwa katika Mohamed na mwenzake (1998).

karaha *ji* maudhi, kero, makuruhu, udhia, maudhiko, usumbufu, uchafu, ginginizo, gingizo, adha, idhilahi, takilifu. (Jumla ya sinonimu ni 12).

Kitomeo **karaha** kimeyaacha maneno 18 ambayo yalikuwa ndani ya kitomeo **madhila** pamoja na neno **madhila** lenyewe lililokuwa neno kuu katika kitomeo hicho. Kwa kulinganisha na kitomeo **madhila** kitomeo **karaha** hakikuingiza neno **madhila** ambalo lilikuwa muhimu sana kwani neno **karaha** limeingizwa kwenye kitomeo **madhila** kama sinonimu .

Utaratibu unaofaa wa uingizaji sinonimu usioleta mashaka ni ule ambao unamwezesha msomaji kuyaona maneno yanayodaiwa kuwa sinonimu katika vidahizo vyote ambavyo ni sinonimu. Baada ya neno kuingizwa kama kitomeo sinonimu zake zitakuwa zinamwongoza mtumiaji wa kamusi kurejea kwenye neno kuu.

Baada ya neno **madhila** kuingizwa na sinonimu zake kuorodheshwa kilichotakiwa kufanywa ni vitomeo vinavyohusiana nalo kuingizwa kwa kulielekea neno hilo. Kwa mfano:

karaha ji taz. madhila.

mzingile ji taz. madhila.

mateso ji taz. madhila.

Hii ingesaidia mambo matatu muhimu:

- (i) Ingeokoa nafasi katika kamusi badala ya kila mara kurudia rudia msururu wote.
- (ii) Ingesaidia kutosahau maneno mengine kama tulivyoona hapo juu.
- (iii) Ingemsaidia msomaji kuuona mshikamano wa maana za maneno.

Sinonimu zilizoorodheshwa katika Mohamed na mwenzake (wameshatajwa 1998) tunaweza kuziweka katika makundi kutegemea uhusiano wa karibu zaidi wa maneno hayo.

Lugha ya Kiswahili ina lahaja zipatazo 18 na hii inawezekana kuwa ndiyo sababu ya kuwa msururu mkubwa wa sinonimu unaotokana na lahaja hizo na kwamba si sinonimu za Kiswahili sanifu.

2.2 Maana Zinazokinzana

Maana za maneno katika kamusi zinapaswa kufafanuliwa kwa wazi zaidi kwani iwapo maana zinazotolewa kwenye kamusi hazikuwekwa wazi zinaweza kuwa chanzo cha sinonimu kutumiwa isivyopasa. Chuwa (1995) anadokeza kuwa katika TUKI (1981) baadhi ya maneno yamepewa maana zinazokinzana kama mifano ifuatayo inavyoonyesha.

- (i) **ushinde** ji 1. ushindi. 2. ushindwaji. TUKI (1981: 306)

- (iii) **mbwende** *ji* 1. nafaka jamii ya maharagwe au fiwi: **kula** ~ (a)
faidi. (b) pata, taabu. 2. -----, TUKI (imeshatajwa uk. 160)

Kwa kuangalia maana za **ushinde** ni dhahiri kuwa zinapingana na za sinonimu zake kwani **ushindi** inakinzana na **ushindwaji**.

Kamusi ambayo maneno yake yamefasiriwa kama hapo juu yanachangia katika kumpotosha mtumiaji kama Neubauer (1984:117) anavyosema:

“Kama watu wengi tunavyofahamu watumiaji wengi wa kamusi wahidiya wakati mwingi hawaridhishwi na matokeo ya utumizi wa kamusi kwa sababu wanapewa maana za mzunguko au kupewa maelezo ambayo hayaeleweki.”

Landau (1984) anasema kuwa kufasiri maneno katika hali ya kutatanisha inawanyima wasomaji kupata maana kamili ya neno, hilo ndilo jambo baya zaidi linaloweza kufanywa na kamusi yo yote ile.

3.0 Kanuni za Uundaji wa Maneno

Kanuni mbalimbali za lugha hutumika kuzalisha maneno mbalimbali. Katika Kiswahili kuna kanuni kadhaa zinazotumiwa kuzalisha maneno aina ya nomino kutokana na vitenzi. Hapa chini kanuni ya unyambulishi itajadiliwa.

3.1 Minyambuliko

Baadhi ya minyambuliko inayoweza kutokea katika vitenzi huzalisha nomino kama katika mifano ifuatayo:

haribu - uharibifu/uharibivu
potoka - upotofu/upotovu
okoka - wokofu/wokovu

Katika mifano ya hapa juu fonimu [*f*] na [*v*] zinaweza kupishana bila kuleta upotofu wa maana yaani zinakuwa katika mpishano huru.

Hata hivyo, mifano ifuatayo hapa chini inaonyesha jinsi fonimu /*ff*/ na /*vv*/ ambazo haziwezi kubadilishana nafasi:

danganya - udanganyifu/*udanganyivu
pofuka - upofu/ *upovu
adili - uadilifu/ * uadilivu
amini - uaminifu/*uaminivu
badili - ubadilifu/ *ubadilivu

batili	- ubatilifu /* ubatilivu.
vumilia	- *uvumilifu uvumilivu
zamia	- *uzamifu uzamivu
badhiri	- ubadhilifu *ubadhilivu

Data hii hapa juu bado haijatuonyesha wazi nini chanzo cha kuwa na [f] na [v] katika kubadili vitenzi kuwa nomino. Kwa kuwa hakuna kanuni mahususi inayojitokeza kwa uwazi basi husababisha baadhi ya watumiaji wa maneno ya namna hii kuyatumia kwa makosa kwani huweza kuchanganya pale panapohitaji kuwa na [f] huwekwa [v] na kinyume chake.

Kitenzi **okoka** kina uwezo wa kuzalisha nomino **wokofu** na **wokovu** lakini kitenzi **okota** chenye muundo wa nje unaofanana na **okoka** yaani katika idadi ya silabi na fonimu hakiwezi kuzalisha nomino zinazofanana na hizo. Kwa kuangalia maneno haya tunaweza kuona kuwa neno **okoka** tayari limefanyiwa unyambulishi yaani limetokana na neno la msingi **okoa**, kitenzi **okota** hili ndilo umbo lake la msingi yaani halitokani na unyambulishi. Hivyo maneno haya yanakutana wakati moja linakuwa kwenye unyambulishi wa hatua ya kwanza na lingine linakuwa bado lipo katika umbo lake la msingi.

Vivyo hivyo kitenzi **potea** kinazalisha nomino **upotevu** lakini kitenzi **sotea** hakizalisha nomino ***usotevu**. Ingawa vitenzi hivi vinaonekana kuwa sawa katika muundo wa nje, lakini katika muundo wa ndani vinatofautiana kwani neno **potea** ndiyo umbo la msingi wakati neno **sotea** ni hatua ya kwanza ya mnyambuliko unaotokana na umbo la msingi la neno **sota**.

Hivyo tunaweza kusema tofauti inayoonyeshwa na maneno **okota** na **okoka**; **potea** na **sotea** zinatokana na kuwa mengine yameingia kwenye kiwango cha unyambulishi kilichofanywa kwa maneno **okoka** na **sotea**.

Mtumiaji asipokuwa makini katika kuzifahamu kanuni zinazotawala mabadiliko ya maneno anaweza kupotoka katika matumizi ya maneno kama haya. Ingawa muundo wa nje wa vitenzi hivi unafanana lakini muundo wa ndani wa vitenzi hivi ni tofauti na ndiyo maana kunakuwa na tofauti katika unyambulishi wake.

4.0 Namna ya Kurekebisha Hali

Watumiaji wengi wa lugha wanapokinza na suala linalohusiana na maana na matumizi ya maneno hukimbilia kwenye kamusi. Hivyo utatuzi wa sababu za upotofu katika uteuzi zinaweza kupatiwa ufumbuzi ndani ya kamusi. Hivyo kwa kiasi kikubwa urekebishaji wa sababu hizo unapatikana au unaweza kupatikana iwapo kamusi zinaweza kusawidiwa kwa umakini zaidi na kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wake.

Uingizaji wa sinonimu ndani ya kamusi ni muhimu kama ilivyodokezwa hapo juu. Mtunga kamusi anapaswa kuchanganua nduni za maneno na hivyo kujua tofauti za msingi kati ya neno na neno kabla ya kutoa uamuzi wa kuwa maneno hayo ni sinonimu kamili au si sinonimu kamili. Hiyo itamsaidia kuyaingiza ndani ya kamusi kwa kuyapa uhusiano na hadhi stahilifu.

Katika kuonyesha sinonimu ndani ya kamusi ni vyema kuwa na maneno machache ambayo yanaonyesha kuwa ni sinonimu kamili na hii itasaidia kupunguza msururu mkubwa wa maneno katika kitomeo yanayodhaniwa kuwa ni sinonimu kamili kumbe wakati maneno mengine yanashirikiana baadhi ya fahiwati tu. Lugha ya Kiswahili inahitaji umakini wa ziada katika kubainisha sinonimu kwani kutokana na lahaja nyingi za lugha ya Kiswahili mtunga kamusi anaweza kuchukua maneno ya vilahaja na kuyaingiza katika Kiswahili kama sinonimu.

Katika kamusi maana za maneno zisionyeshe ukinzani au maana za neno moja zisiwe na fahiwati ya chanya na hasi kwa wakati mmoja katika jamii moja ya watumiaji wa lugha. Hii itasaidia katika kuepusha kuwachanganya watumiaji.

Minyambuliko ya maneno katika kamusi ionyeshwe kwa uwazi na kufasiriwa ili mtumiaji kamusi asipate shida ya kufanya fasiri zake mwenyewe kwa kutegemea tu fasiri ya msingi iliyotolewa kwenye kitomeo kwani wakati mwingine maana ya kinyambuo inaweza kukengeuka maana ya msingi.

Kanuni mbalimbali za uzalishaji maneno zinapaswa kudokezwa ndani ya kamusi ili kumsaidia mtumiaji anapokinza aweze kujinasua kwa kufahamu kuwa kwa kanuni fulani anaweza kuunda neno la aina fulani.

5.0 Hitimisho

Makala haya yamekusudiwa kudokeza baadhi ya sababu za uteuzi potofu wa sinonimu zinazotumiwa na wasemaji na waandishi wa Kiswahili. Tumeona kuwa kutozingatia mahusiano ya sinonimu na vivuli vya maana kunaweza kupotosha matumizi ya baadhi ya maneno kwa kudhani kuwa ni sinonimu wakati maneno hayo si sinonimu. Kutokuwa makini katika kanuni mbalimbali za uundaji wa maneno ni moja ya vyanzo vya matumizi potofu katika Kiswahili. Misururu mirefu ya sinonimu nayo huwachanganya watumiaji wa Kiswahili kwani lugha haionyeshi utajiri kwa kuwa tu na maneno mengi yenye uhusiano wa karibu.

Makala pia imeonyesha namna ya kurekebisha hali hiyo kwa kuonyesha kuwa mtunga kamusi anapaswa kuwa makini katika kubainisha sinonimu ndani ya kamusi ili kuifanya kamusi iweze kumsaidia zaidi mtumiaji kutotumbukia katika matumizi potofu ya sinonimu za Kiswahili.

MAREJEO

- Chiduo, E.K. (1997) 'Synonymy in the Swahili Standard Dictionary'. Unpublished Doctoral Dissertation, T.C. New York. Columbia University.
- Chuwa, A.R. (1995) "Lugha, Kioo cha Jamii" Katika Y. M. Kihore na A.R. Chuwa, *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja*, Dar es Salaam: TUKI, UDSM.
- Hartmann, R.R.K. (Ed) (1993) *Lexicography: Principles and Practice*, London: Academic Press.
- Jackson, Howard (1988) *Words and Their Meaning*. London: Longman.
- Landau, Sidney (1984) *Dictionaries: the Art and Craft of Lexicography*. New York: Charles Scribners' Sons.

- Lyons, J. (1968) *Introduction to Theoretical Linguistics*. London: Cambridge University Press.
- Mohamed A. Mohamed na mwenzake. 1998. *Kamusi ya Visawe*. Nairobi: East African Education Publishers.
- Singh Ram Adhar. (1982) *An Introduction to Lexicography*. Central Institute of Indian Languages. India.
- TUKI. (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- TUKI. (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la II*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Weinreich, Uriel. (1980), *On Semantics*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.